https://maktaba.tetea.org

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

**686** **VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2022**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma maelekezo **yote** kwenye kijitabu chako cha kujibia.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** kwenye chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Kwa kutumia mifano, eleza kwa kifupi manufaa manne ya kutumia mbinu ya michezo katika kukuza lugha kwa mtoto.

2. Kwa kutumia hoja nne, fafanua kwa kifupi athari zinazoweza kutokea endapo mtoto atashindwa kuonesha mwitikio chanya katika tendo la ujifunzaji.

3. Fafanua kwa kifupi, mambo manne ambayo mwalimu anapaswa kuyazingatia ili kukuza lugha kwa mtoto.

4. Eleza kwa kifupi, faida nne za mwalimu kutumia mbinu ya maswali na majibu kumfundishia mtoto stadi za mawasiliano.

5. Ni mambo gani anayoweza kufanya mwalimu na kusababisha mtoto kupoteza umakini wa kusikiliza awapo darasani? Fafanua kwa kifupi mambo manne.

6. Eleza kwa kifupi namna vifaa vifuatavyo vinavyotumika kufundishia stadi za mawasiliano kwa mtoto:
   (a) Runinga.
   (b) Kanda za kaseti.

7. Kwa kutumia hoja nne, bainisha makosa ambayo mwalimu anaweza kumrekebisha mtoto wakati wa usomaji wa maneno au sentensi.

8. Fafanua kwa kifupi faida za kutumia onesho mbinu katika kufundishia watoto wa Elimu ya Awali.

9. Eleza faida nne za kuandaa mapema zana za kufundishia na kujifunzia stadi ya kusoma.

10. Kwa kutumia hoja nne, chambua kwa kifupi manufaa ya kutumia orodha hakiki kama zana ya upimaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za awali za kusoma.

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. "Mwalimu anayefundisha stadi za masimulizi hukutana na changamoto nyingi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji." Kubaliana na kauli hii kwa kutumia hoja tano.

12. Kwa kutumia mifano, eleza manufaa anayoyapata mtoto katika ujifunzaji wa lugha. Tumia hoja tano.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

13. Kwa kutumia mfano kwa kila moja, fafanua hatua tano za kufuata katika ufundishaji wa kuandika herufi za Kiswahili katika Darasa la Awali.

14. Ili kuepuka changamoto zinazoweza kujitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu hana budi kufanyia majaribio zana za kufundishia na kujifunzia kabla ya kuingia darasani. Chambua faida sita za kufanyia majaribio zana za kufundishia na kujifunzia Stadi ya Kuandika.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org